

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA HALMASHAURI

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ilipanga kukusanya na kutumia jumla ya **Tshs. 50,743,721,389.00**. Ikiwa, Mishahara **Tshs. 36,867,322,280.00**, Ruzuku toka Serikali Kuu na Wahisani **Tshs. 7,682,348,617.00**, **Tshs. 2,305,938,492.00** fedha za matumizi mengineyo (OC) na **Tshs. 3,388,212,000.00** Mapato ya ndani (Ikiwa mapato halisi ni **Tshs. 3,534,421,000.00** na mapato mengineyo ni **Tshs. 353,791,000.00**).

Katika kipindi cha 2020/2021, Halmashauri imeweza kukusanya jumla ya **Tshs. 41,539,338,693.00** sawa na 81.9% ya makadirio, ambapo mapato toka vyanzo vya ndani ni **Tshs. 4,061,865,273.00** sawa na 104% ya makadirio, Miradi ya Maendeleo **Tshs. 5,850,792,288.00** sawa na 76% ya makadirio, Mishahara **Tshs. 30,203,041,299.00** sawa na 82% na matumizi mengineyo (OC) **Tshs. 1,423,639,833.00** sawa na 62% ya makadirio.

Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiria kukusanya na kutumia jumla ya **Tshs. 3,888,212,000.00** kutoka vyanzo vya ndani (Own Source – Mapato halisi **Tsh. 3,534,421,000.00** na Mapato Mengineyo **Tsh. 353,791,000.00**). Jumla ya Makusanyo ya mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ni **Tshs. 4,061,865,273.00** sawa na **asilimia 104**.